

# **Monitoring Learner Achievement at Primary School Level in Kenya**

## **Darasa la 7**

**JINA:** \_\_\_\_\_

**NAMBARI YA USAJILI:** \_\_\_\_\_

**MAAGIZO KWA WANAFUNZI  
SOMA MAAGIZO YAFUATAYO KWA MAKINI.**

1. Kijitabu hiki kina maswali **50**.
2. Hakikisha ya kwamba umeandika jina lako na nambari yako ya usajili.
3. Umepewa muda wa **saa 1 na dakika 40** kujibu maswali yote.
4. Katika baadhi ya maswali umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi A, B, C, D, Ni jibu MOJA tu kati ya hayo manne ambalo ni sahihi. Chagua jibu hilo.
5. Chora kiduara au pigia mstari herufi ambayo ndilo jibu lako.

**Mfano**

**21.** Chagua jibu lenye ala za muziki pekee.

- A. filimbi, udi, mvukuto, chapuo  
 B. njuga, tari, kinubi, fidla  
 C. harimuni, marimba, msondo, malemba  
 D. siwa, zeze, upatu, nembo

Jibu sahihi ni **B**. Jibu hili ndilo lililochorewa kiduara.

6. Piga mstari au chora kiduara kwenye jibu moja tu.
7. Jibu maswali mengine kulingana na maagizo yaliyotolewa.

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI**

**JEDWALI LA ALAMA**

<b>SWALI</b>	1	2	3	4	5	6	7	8	9	10	11	12	13	14	15
<b>UPEO</b>	1	1	1	1	1	1	1	1	1	1	1	1	1	1	1
<b>ALAMA</b>															

<b>SWALI</b>	16	17	18	19	20	21	22	23	24	25	26	27	28	29	30
<b>UPEO</b>	1	1	1	1	1	1	1	1	1	1	1	1	1	1	1
<b>ALAMA</b>															

<b>SWALI</b>	27	28	29	30	31	32	33	34	35	36	41	42	43	44	45
<b>UPEO</b>	1	1	1	1	1	1	1	1	1	1	1	1	1	1	1
<b>ALAMA</b>															

<b>SWALI</b>	37	38	39	40	41	42	43	44	45	46	47	48	49	50	<b>JUMLA</b>
<b>UPEO</b>	1	1	1	1	1	1	1	1	1	1	1	1	1	1	50
<b>ALAMA</b>															

Soma kifungu kifuatacho. Kina nafasi **1** mpaka **10**. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne. Chagua jibu lifaaloo **zaidi** kati ya yale manne uliyopewa.

Haki za watoto ni suala **1** kushughulikiwa. Watoto **2** wanafaa **3** haki **4**. Wana haki ya kucheza na **5** na kupata elimu. **6**, wanastahili nzuri kupata lishe bora **7** mavazi na mahali pa kuishi. Walezi wana **8** kuhakikisha kuwa kila mtoto anapata haki **9**. **10** wanahatarisha maisha ya watoto.

- |     |                 |                 |                 |                |
|-----|-----------------|-----------------|-----------------|----------------|
| 1.  | A. linapohitaji | B. linalohitaji | C. linayohitaji | D. linaohitaji |
| 2.  | A. wote         | B. sote         | C. nyote        | D. yote        |
| 3.  | A. kutimiziwa   | B. kutimizia    | C. kutimizwa    | D. kutimizika  |
| 4.  | A. kwao         | B. yao          | C. lao          | D. zao         |
| 5.  | A. nyingine     | B. wengine      | C. mengine      | D. jingine     |
| 6.  | A. Isitoshe     | B. Ilhali       | C. Ikiwa        | D. Isipokuwa   |
| 7.  | A. .            | B. !            | C. ,            | D. ?           |
| 8.  | A. matarajio ya | B. jukumu la    | C. shughuli ya  | D. lengo la    |
| 9.  | A. hiyo         | B. hilo         | C. hizo         | D. hivyo       |
| 10. | A. Wakipuuza    | B. Wakapuuza    | C. Wanapuuza    | D. Wamepuuza   |

Kutoka swali la **11** mpaka **15**, chagua jibu sahihi.

- 11.** Chagua neno lenye silabi **tano**.  
A. atasoma      B. mvumilivu      C. orodha      D. ingawa

- 12.** Jaza mapengo kwa maneno sahihi.

\_\_\_\_\_ mvua ilinyesha \_\_\_\_\_ hakukuwa na mafuriko.

- A. Bali, tena      B. Ilhali, mno  
C. Japo, sana      D. Lau, zaidi

- 13.** Ni sentensi ipi **isiyo** katika kauli ya kutendea?

- A. Toma alichotea maji kwa Sudi.  
B. Julia aliandikia kalamu ya wino.  
C. Tina anamfumia mama mkeka.  
D. Koto amerejea nyumbani kwao.

14. Rafiki yako anacheza karibu na kidimbwi cha maji huku akijua ni hatari. Chagua kauli ambayo utatumia kumuonya.
- A. Tafadhali usijipalie makaa.
  - B. Chunga, utakula mwande.
  - C. Tahadhari, utamwaga unga.
  - D. Jamani utajifanyia inda.
15. Chagua sentensi inayoonyesha masharti.
- A. Susa alikuwa akimsaidia babu nyumbani.
  - B. Tata alikipaka rangi kijumba chake kikapendeza.
  - C. Nina akipalilia mimea vizuri atapata mavuno tele.
  - D. Kanda alikihofadhi cheti chake ndani ya sanduku.

*Kutoka swali la 16 mpaka 30, jibu swali kulingana na maagizo.*

16. Panga maneno haya kama yanavyofuatana katika kamusi. maktaba, maabara, maegesho, mabati
- 
- 

17. Nomino **nyuta, kucha na mbao** ziko katika ngeli gani?
- 

18. Andika sentensi ifuatayo katika usemi halisi.  
Dereva alituambia tufunge mikanda ya usalamu.
- 
- 

19. Rafiki yako amepiga picha nzuri kinyume na matarajio yako. Utatumia kihisishi gani?  
\_\_\_\_\_ umepiga picha nzuri hivi?
- 

20. Onyesha aina ya neno lililopigiwa mstari katika sentensi ifuatayo:
- Gari liliwuwa kando ya barabara.
- 
21. Andika sentensi ifuatayo upya kulingana na maagizo.  
Nilimkuta Juma ambapo unapitia mto Salama.  
**Anza kwa:** Unapopita Mto Salama
- 
22. Kanusha sentensi ifuatayo:  
Mlezi aliwanunulia watoto wake majarida mjini.
- 
23. Andika sentensi ifuatayo katika wingi. Chungwa ambalo mtoto huyu anakula limeiva.
- 
24. Panga maneno yafuatayo kuunda sentensi sahihi.  
Nyumbani darasa kisha wanafunzi lao walifagia wakaenda
- 
25. Andika sentensi ifuatayo katika udogo:  
Mlango wa kuingia kwake unapendeza.
-

- 26.** Maana ya, **Biko alitutangazia gazeti hilo** ni, “Biko alitumia gazeti kutoa habari kutuhusu.”

Maana nyingine moja ya sentensi hii ni:

---

---

- 27.** Koli anataka kwenda kutazama mechini ya kandanda, atatoa \_\_\_\_\_ kama malipo ili aruhusiwe kuitazama. Akitaka kusafiri kwa gari atalipa nauli.

- 28.** Andika katika tarakimu.  
elfu mia nane, mia nane na tatu

---

---

- 29.** Ndugu yako anapoenda kulala utamuaga kwa kumwambia \_\_\_\_\_.

- 30.** Rafiki yako alizaliwa mwongo mmoja uliopita. Rafiki yako ana umri wa miaka \_\_\_\_\_.

---

Moja kati ya mambo ya kimsingi ambayo binadamu anastahili kufanya ili kudumisha afya ni usafi wa kibinafsi. Mtu anayezingatia usafi wa kibinafsi huhakikisha kwamba ameosha vifaa na mavazi anayotumia, na kwamba ameoga mara kwa mara ili kuutunza mwili wake. Usafi wa kibinafsi humwepusha mtu na magonjwa yanayosababishwa na vimelea kama vile funza na viroboto.

Baadhi ya watu hupuuza usafi wa sehemu nyingine za mwili. Si ajabu kuwapata watu hawa wakinawa uso asubuhi ili kuondoa matongo kwenye macho, na kuoga baada ya shughuli za kutwa ili kuondoa jasho mwilini, lakini wakapuuza usafi wa kinywa.

Kinywa ni sehemu ya uso ambayo huhifadhi sehemu muhimu za mwili kama vile meno na ulimi. Kwa hivyo, hatuna budi kukitunza kinywa chenyewe ili sehemu hizi muhimu ziweze kusetirika. Je, umewahi kuwazia umuhimu wa meno? Mbali na kumpa mtu tabasamu la kuvutia na mvuto wa kijumla wa sura, meno humsaidia binadamu kukitafuna chakula kabla ya kukimeza. Mtu mwenye meno **yaliyodhoofika** hushindwa kula vyema. Hivyo basi kila binadamu anastahili kuyatunza meno yake, lau sivyo atakosa kufaidi utamu wa vyakula kama vile pure, nyama na miwa.

Utunzaji wa meno unahitaji uwajibikaji wa kibinafsi. Ni muhimu kupiga mswaki angaa mara mbili kwa siku. Hili litakusaidia kuondoa ugaga unaoota juu ya meno na uchafu kwenye ulimi. Zaidi ya hayo, unapojenga mazoea ya kusugua meno mara kwa mara unazuia kuenea kwa viini ambavyo huyafanya meno kuoza na kukifanya kinywa chako kitoe harufu mbaya. Hali kadhalika, lishe bora ni njia muhimu ya kutunza afya ya kinywa. Mathalan, juisi ya miwa husaidia kuzuia meno kuoza. Utafunaji wa miwa huimarisha meno na mifupa. Karoti nayo huipa mifupa na meno kalisi ambayo ni madini muhimu katika kuyaimarisha. Vyakula vyenye vitamini C kama vile mchicha na machungwa huimarisha ufizi na meno. Ukosefu wa vitamini C husababisha kuvimba kwa ufizi na kutokwa na damu. Ugonjwa huu huitwa hijabu. Ikumbukwe pia kwamba ulaji wa vyakula vyenye sukari nyingi huathiri afya ya meno. Vyakula kama vile biskuti na pipi huyafanya meno kuwa na matundu ambayo ni mazingira mufti ya kuzaana kwa viini. Viini hivi huyafanya meno kuoza na hatimaye kung'oka. Afya ya kinywa na meno huhusu pia utunzaji wa ufizi. Ufizi ni nyama inayoshikilia meno kinywani. Ufizi huweza kuharibiwa kwa vitendo kama vile kuingiza vijiti katikati ya meno ili kuondoa mabaki ya vyakula, kung'ata vitu vigumu na kusugua meno kwa mswaki wenye vijiti visivyofaa.

Walisema wasemao kwamba ukiona vyaelea juu vimeundwa, nako kuwa na meno imara hutegemea juhudzi za mtu binafsi. Ni jukumu la kila mtu kuhakikisha kwamba ameepuka vitendo ambavyo vinahatarisha afya ya kinywa chake. La muhimu zaidi anastahili kumwona daktari wa meno mara kwa mara ili kupata ushauri ufaao kuhusu utunzaji bora wa meno.

- 31.** Kulingana na aya ya **kwanza**:
- Watu wanaofua nguo hawapatwi na magonjwa.
  - Afya ya mwili hutegemea usafi wa mtu.
  - Mtu anayevaa nguo nyingi kwa siku ana afya.
  - Wadudu huwavamia watu wasiowazia magonjwa.
- 32.** Kulingana na aya ya **pili**, watu wengi
- husumbuliwa na uchafu asubuhi.
  - huthamini usafi baada ya shughuli ngumu.
  - huzingatia usafi wa baadhi ya sehemu za mwili.
  - husahau uchafu ulio kwenye meno.
- 33.** Chagua jibu **lisilo sahihi** kulingana na aya ya **tatu**. Meno
- humsaidia mtu kumeza chakula haraka.
  - humwezesha mtu kuonyesha hisia zifaazo.
  - humjengea mtu sura ya kupendeza.
  - humrahishisha mtu kazi ya kutafuna chakula.
- 34.** Aya ya **tatu** inadhihirisha kwamba:
- Kinywa huyafanya meno kuwa kiungo muhimu.
  - Binadamu akitunza meno yake atafurahia utamu wa chakula.
  - Chakula kizuri humfaidi zaidi mtu mwenye meno imara.
  - Manufaa ya utunzaji wa meno humfanya mtu kufikiri sana.
- 35.** Upigaji mswaki huwa na manufaa yafuatayo **isipokuwa**:
- Kuondoa ugaga unaoota kwenye meno.
  - Kuzuia kuenea kwa viini.
  - Kuzuia harufu mbaya ya kinywa.
  - Kupata madini ya kalisi.
- 36.** Kulingana na aya ya **nne**, ni kauli ipi inayoonyesha kwamba tabia ya mtu huathiri hali yake ya afya?
- Unapojenga mazoea ya kusugua meno unazuia kuenea kwa viini.
  - Juisi ya miwa husadia kuzuia meno kuoza.
  - Karoti nayo huipa mifupa na meno kalisi nyingi.
  - Vyakula kama vile biskuti na pipi huyafanya meno kuwa na matundu.
- 37.** Chagua msimamo wa mwandishi katika aya ya **mwisho**.
- Kuimarika kwa afya hutegemea uhusiano kati ya mtu na daktari wake.
  - Utendakazi wa viungo vya mwili hutegemea jinsi mtu anavyovitunza viungo hivyo.
  - Kila binadamu anastahili kuhakikisha kwamba anavithamini viungo vya mwili wake.
  - Idadi kubwa ya watu inapaswa kupewa maelekezo yafaayo kuhusu afya.
- 38.** Maana ya **yaliyodhoofika** kulingana na kifungu ni yenyе:
- kukosa mvuto
  - mianya mingi
  - kukosa nguvu
  - vitamini chache
- 39.** Kulingana na kifungu, kauli **hatuna budi** inamaanisha:
- tunalazimika
  - tunatambua
  - tumezoea
  - tumeamini
- 40.** Kifungu kimeonyesha kwamba mtu asipodumisha usafi huvamiwa na funza na viroboto. Andika vimelea wengine wawili ambao hawajatajwa kwenye kifungu ambao mtu anayezingatia usafi wa kibinagsi anaweza kuwaepuka.

*Soma hadithi ifuatayo kisha ujibu swal la 41 mpaka 50.*

Ilikuwa wakati wa likizo. Kai alikuwa amemtembelea babu yake mashambani. Siku hiyo Kai alimpata babu amekalia kigoda kilichokuwa chini ya mti. Babu alikuwa anasoma gazeti la *Msema Kweli*. Ubavuni mwake mlikuwa na sahani ambayo bila shaka ilikuwa imetumiwa kwa chakula cha mchana.

“Shikamoo babu!” Kai alimwamkua babuye.

“Marahaba mjukuu wangu, hujambo? Njoo uketi nami hapa.” Babu alimkaribisha Kai.

Kai aliketi kwenye mkeka uliokuwa karibu na babu.

“Babu unasoma nini?” aliuliza Kai huku akitazama picha ya kuvutia iliyokuwa kwenye ukurasa wa kwanza wa gazeti hilo.

“Ah! Mjukuu wangu, ni haya mambo yenu yasiyoisha kushangaza.”

“Babu, kwa nini yawe ya kushangaza? Kwani ulipokuwa na umri kama wangu mambo hayo uyasemayo hayakuwapo?”

“Mjukuu wangu, si kwamba siku zetu hakukuwa na mambo. Lakini haya ya kijana huyu kwenye gazeti hili! Sijui kwa nini hamjishughulishi kuwafahamu watu wa ukoo wenu! Inaonekana mnajizika kwenye vitabu na kusahau elimu ya ukoo. “Siku zetu,” aliendelea babu huku akilifunga gazeti lake na kumtazama Kai, “wanajamii wote waliishi kama familia moja. Niliwafahamu ya akina babu, nyanya, mjomba, shangazi, amu, mama mkubwa, mama mdogo pamoja na watoto wao wote. Mngekuwa kama sisi bila shaka aibu iliyompata kijana huyu isingempata.”

“Lakini babu,” alisema Kai huku akitaka kumwelekeza babu kwenye mkondo mwengine wa mazungumzo, “hivi siku zenu mlikuwa mkipata vipi taarifa? Nasikia siku hizo hakukuwa hata na redio!” “Ah! Mjukuu wangu, umedanganyika. Mimi nilipozaliwa nilipata kuwa kulikuwa na magazeti na televisheni. Babangu alikuwa na kiredio chake ambacho daima kilikesha juu ya kochi pale sebuleni. Ndicho kilichokuwa jogoo wa kutuamsha. Na usidhani ni kiredio tu, alikuwa pia na televisheni, ila yake ilikuwa tofauti na hizi zenu mlizozoea, lakini ilitupa habari na burudani tosha. Hakika sisi na majirani wetu tulijumuika sebuleni mwa baba kutazama televisheni baada ya kazi ya kutwa.”

“Babu, je, mlipata habari kuitia magazeti na televisheni tu? Siku hizi sisi hupata habari kuitia kwenye simu. Hata hili gazeti ulisomalo limo kwenye simu hii yangu. Nililisoma asubuhi hata kabla ya kuja hapa.”

“Aa babangu, simu zilikuwapo, ila zilikuwa na tofauti kidogo tu na hizi zenu. Zetu zilikuwa kubwa na ziliwekwa mezani ndani ya chumba. Hatukuwa na nafasi ya kuzunguka nazo jinsi mnavyofanya siku hizi.”

“Babu!” alisema Kai huku akichekacheka, “tofauti si ndogo? Huwezi kulinganisha simu inayokuwezesha kutuma baruapepe na kusakura habari muhimu kutoka kwenye mtandao na hizo zenu za zamani. Hizi ni bora zaidi. Zinabeba elimu yote ya vitabuni. Siku hizi hatuna hata haja ya kwenda kwenye maktaba kuketi huko. Unaweza kujisomea hapa hapa kwenye kivuli cha mti huu. Hujui hata akina Mutuma wanafanya mitihani kuitia vifaa kama hiki?”

“Sikatai kwamba vifaa hivi vyenu vya kisasa vimerahisisha maisha. Linalonisumbua ni kwamba mmekuwa watumwa wa vifaa hivi. Siku ngapi nimewaonya binamu zako dhidi ya kuchenza michezo kwenye mitandao kupita kiasi? Siku ngapi nimemwonya kaka yako dhidi ya kupiga soga na wenzake kwenye simu wakati wa maakuli? Si juzi tu niliposikia ukemi kutoka kwa Mzee Maarifa, nyumba nzima imejaa moshi, chakula kimeungua jikoni huko watoto wamepotelea kwenye simu zao?”

“Babu, hiyo ilikuwa bahati mbaya tu,” alisema Kai huku akitaka kuinuka kutoka kwenye mkeka, “Na iwe hiyo bahati mbaya. Ila nataka ujue kwamba hiyo ilikuwa ajali ambayo ingekuwa na kinga.

Pamoja na manufaa ya vifaa hivi, mnahitaji kuvitumia kwa nidhamu na tahadhari; lau sivyo mtakuja **kujiuma vidole**.”

- 41.** Kulingana na aya ya **kwanza**:
- Kai alipenda kumtembelea babu wakati wa likizo.
  - Kai alipofika babu alikuwa amekula chakula cha mchana.
  - Babu alipenda kusomea gazeti chini ya mti.
  - Babu alipomwona Kai aliinuka kwenye kigoda.
- 42.** Ni jambo gani linaloonyesha kuwa Kai ana heshima?
- Anamwamkua babu yake.
  - Anamuuliza babu anachosoma.
  - Anamtembelea babu yake mashambani.
  - Anainuka huku babu akizungumza.
- 43.** Babu anashangazwa na jambo gani katika gazeti analolisoma? Vijana
- kupuuza haja ya kujua wanaohusiana nao kwa damu.
  - kucheza michezo nyumbani kupita kiasi.
  - kuacha chakula kuungua wakishughulika kwenye simu.
  - kuwaza kwamba wazee wao hawakuja umuhimu wa radio.
- 44.** Kifungu kimebainisha kwamba elimu ya ukoo
- huturahisishia kuwepo kwa elimu ya vitabu.
  - hutuongezea pamoja kutazama televisheni.
  - hutuongezea ujasiri wa kuuliza maswali.
  - hutuwezesha kufahamu jamaa zetu.
- 45.** Kwa mujibu wa kifungu, chagua orodha inayoonyesha vyombo viliviyotumiwa kutoa habari enzi za babu.
- magazeti, jogoo, televisheni
  - jogoo, baruapepe, vitabu
  - vitabu, radio, baruapepe
  - televisheni, magazeti, radio
- 46.** Kauli zifuatazo zinaonyesha ucheshi wa babu **isipokuwa** masimulizi kuhusu
- kiredio chao kukesha kochini na kuwa jogoo wa kuwaamsha.
  - babu na majirani kujumuika sebuleni kutazama televisheni.
  - ushauri dhidi ya kupiga soga kwenye simu wakati wa maakuli.
  - simu kubwa isiyobebeka iliyowekwa mezani ndani ya chumba.
- 47.** Kulingana na kifungu, ni jambo lipi linalooyesha kuwa vijana ni watumwa wa mtandao?
- Kutokuwa na nidhamu wanaposhiriki mazungumzo
  - Kutokuwa makini katika kazi za nyumbani
  - Kutosoma magazeti mara kwa mara
  - Kutojali mahusiano baina yao na majirani
- 48.** Kauli, **kujiuma vidole**, imetumia tamathali gani ya usemi?
- sitiari
  - tashihisi
  - nahau
  - chuku
- 49.** Kwa mujibu wa kifungu, babu anatoa ushauri gani kuhusu matumizi ya vifaa vya mawasiliano?
- 
- 
- 
- 50.** **Mjukuu na babu** ni majina ya kiukoo. Taja majina mengine mawili ya kiukoo hayajatajwa katika hadithi.
- 

**HUU NDIO UKURASA WA MWISHO ULIOPIGWA CHAPA.**